

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



TAARIFA KWA UMMA

30 Novemba, 2018

**UTARATIBU MPYA WA KULIPIA HUDUMA ZA TFDA KUPITIA MFUMO WA
SERIKALI WA GePG**

1. Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) inapenda kuwafahamisha wateja wake na wananchi kwa ujumla kuwa, kuanzia tarehe 1 Desemba 2018, itaanza rasmi kutumia mfumo wa malipo wa Serikali wa kieletroniki (Government e-Payment Gateway-GePG) kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348.
2. Malipo yote kwa huduma zitolewazo na TFDA yatafanyika kwenye akaunti za Mamlaka na kwa kuzingatia namba maalum ya utambuzi (Payment Control Number) zinazooneshwani kwenye ankara kifani (proforma invoice).
3. Huduma itatolewa baada ya malipo kukamilika kwa mujibu wa Kanuni za Ada na Tozo za mwaka 2005 kama zilivyorekebishwa mwaka 2015.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana nasi kupitia anuani ifuatayo;

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA),
Mtaa wa Mwanza, Block T,
Kiwanja Na. 6, S.L.P 1253,
Dodoma,Tanzania.**

Simu (Landline): +255 26 320156
Simu (Mobile):+255 658 445222/+255 685 70173
Barua pepe: info@tfda.go.tz
Tovuti: www.tfda.go.tz